GRPS my choice®
Grand Rapids Public Schools

HERE COMES THE BUS

Here Comes the Bus ni nini?

Here Comes the Bus ni programu ya vifaa vya mkononi na tovuti ya kutumika kirahisi inayowawezesha wazazi na walezi walitazame kwa muda halisi eneo la basi ya shule ya mtoto wao kwenye kompyuta, tableti, au simutamba. Kwa ziada, arifa za baruapepe na taarifa za msukumo zinawasaidia wazazi wawapeleke wanafunzi wao kwenye kituo cha basi kwa wakati mwafaka.

Programu hii inaweza kutazamwa kwenye simutamba yoyote (Apple iPhone, Samsung Galaxy, BlackBerry, na kadhalika) kwa kuingiza kitambulisho cha mwanafunzi na nambari ya akaunti iliyopewa na wilaya ya shule.

Kuunda Akaunti:

Ili kuunda akaunti ya Here Comes the Bus (HCTB) kwa kutumia programu, fuata hatua hizi kwenye kurasa zifuatazo.

Tumia msimbo huu wa tarakimu tano uwe msimbo wa wilaya ya shule wa GRPS: 29651

Kuwa na kitambulisho cha mwanafunzi uliye naye maanani, ikiwa unakijua. Ikiwa hukijui, kutakuwa kuna maagizo baadaye kuhusu hatua za jinsi ya kukipata kutoka kwenye shule yako.

Ili kuanza, tafuta “Here Comes the Bus” ndani ya Duka la Programu la kifaa chako

Apple App Store: https://apps.apple.com/us/app/here-comes-the-bus/id981902595

Google Play Store: https://play.google.com/store/apps/details?id=com.synovia.herecomesthebus&hl=en_US&gl=US



1 **Pakua na sakinisha programu ya** *Here Comes the Bus* kutoka kwenye Apple App Store au Google Play.



2 Unapoifungua programu kwa mara ya kwanza, utaonyeshwa skrini hii.

Gusa "Sign Up" kwenye sehemu ya chini ya ukurasa.



3 Skrini hii itajitokeza.

Gusa "Continue".

4 Utaambiwa utoe msimbo wa wilaya yako ya shule.

Gusa "I Have the Code".



5 Skrini ya Unda Akaunti Yako itajitokeza.

Charaza anwani yako ya baruapepe, jina la kwanza na mwisho, **na Ingiza 29651 iwe Msimbo wa Wilaya ya Shule.**

Gusa "Continue".



6 "Grand Rapids Public Schools" inafaa kujitokeza ndani ya kisanduku.

Ikiwa ni sahihi, **gusa "Confirm".**



7 Skrini ya Nenosiri itajitokeza.

Charaza nenosiri ambalo ungependa kulitumia kwa programu ya Here Comes the Bus ndani ya sehemu za Nenosiri na Rudia Nenosiri.*

Gusa "Confirm Password".

*Dokezo: Unaweza kuchagua "SHOW" ikiwa ungependa kuthibitisha vibambo ulivyoingiza. Nenosiri lako linahitaji kuwa na vibambo 8 hadi 16. Na lijumuishe herufi kubwa na ndogo na angalau nambari moja na kibambo maalum

8 Utashukuriwa kwa kujisajili kwenye *Here Comes the Bus.*



9 Fungua baruapepe uliyotumiwa kutoka kwa noreply@synovia.com. **Gusa "Activate My Account."**

Utapelekwa hadi kwenye tovuti ya *Here Comes the Bus*, lakini unaweza kuumaliza mchakato wa kuunda akaunti ndani ya programu.



10 Ikiwa uliiacha programu wazi, unaweza kubofya **"Login".**

Ikiwa sivyo, unapofungua programu, utaonyeshwa skrini ya kuingia.

Charaza anwani yako ya baruapepe, msimbo wa wilaya ya shule (29651), na nenosiri.

Gusa "Login".



11 Utadokezwa uongeze maelezo ya mwanafunzi uliye naye.

Ikiwa huna nambari ya kitambulisho ya mwanafunzi uliye naye, **gusa "Need Your Student ID?"**

Ikiwa unayo, ruka chini hadi kwenye hatua ya 14.



12 Maagizo kuhusu jinsi ya kupata nambari ya kitambulisho ya mwanafunzi uliye naye itajitokeza.

Baada ya kufuata maagizo hayo na kukipata kitambulisho, **gusa "Continue".**



13 Skrini ya Maelezo ya Mwanafunzi, iliyoonyeshwa kwenye hatua ya 11, itajitokeza tena.

Charaza kitambulisho cha mwanafunzi na jina la mwisho la mwanafunzi uliye naye.

Gusa "Add Student".



14 Vituo ambavyo idara ya usafiri imemuingizia mwanafunzi uliye naye vitajitokeza. **Ikiwa ni sahihi, gusa "Proceed" na ruka chini hadi kwenye hatua ya 16.**

Ikiwa si sahihi, gusa "I Need Help".



15 Maagizo kuhusu jinsi ya kuifahamisha idara ya usafiri kuwa ina vituo visivyo sahihi kwenye faili yatajitokeza. Itabidi wasahihishe hali hii.

Baada ya wao kufanya hivyo, gusa "Continue" kwenye skrini hii.



16 Kiduara chako cha arifa kitajitokeza kwenye ramani. Hili ni eneo la duara linalozunguka kituo cha basi cha mwanafunzi uliye naye—basi inapoingia kwenye kiduara ndipo utakapopokea arifa kwa baruapepe au taarifa ya msukumo, ikiwa umechagua kupokea hiyo.

Gusa "Continue".

17 Utaona ujumbe wa kufaulu—mwanafunzi uliye naye ameongezwa kwenye akaunti yako! **Unaweza kugusa "Add Another Student" na kurudia mchakato huu ikihitajika. Ikiwa umemaliza kuongeza wanafunzi, gusa "Complete".**



18 Utadokezwa uingize jina la kifaa chako, kama vile "Elizabeth's S8."

Ingiza Jina la Kifaa na gusa "Save".



19 Skrini ya mwanzo ya *Here Comes the Bus* itajitokeza.